Namba ya Mtahiniwa _____

Jina la shule: _____

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA JIJI LA DAR ES SALAAM

MTIHANI WA UTAMILIFU

DARASA LA SABA - APRILI, 2026

01 KISWAHILI

Muda: Saa 1:40 **Tarehe: .....**

MAELEKEZO

1. Karatasi hii ina sehemu **A, B** na **C** zenye jumla ya maswali **Sita (6)**
2. Jibu maswali **yote** katika nafasi uliyopewa.
3. Majibu **yote** yaandikwe katika karatasi hii.
4. Majibu **yote** yaandikwe kwa kalamu yenye wino wa **bluu** au **mweusi**.
5. Andika kwa usahihi **Namba yako ya Mtihani na Jina la Shule** kwenye sehemu ulizopewa.
6. Simu za mikononi na vifaa vingine visivyohitajika **haviruhusiwi** katika chumba cha mtihani.

KWA MATUMIZI YA MTAHINI TU		
Namba ya Swali	**Alama**	**Saini ya Mhakiki**
1		
2		
3		
4		
5		
6		
Jumla		

CamScanner

SEHEMU A: (Alama 20)

1. Sikiliza kwa makini habari utakayosomewa na Msimamizi kisha jibu kipengele cha (i) – (v) kwa kuchagua herufi ya jibu sahihi. 3

i) Kijana aliyeitwa jina la Ranginyingi alikuwa anaishi na nani?
(a) Baba na mama (b) Shangazi yake (c) Jirani yake
(d) Peke yake (e) Babu yake [ ]

ii) Ranginyingi alikuwa na uwezo wa kipekee wa namna gani?
(a) Kuwa na rangi nyingi (b) Kujibadilisha rangi (c) Kuwa mweupe
(d) Kujikondesha (e) Kuwa na rangi chache [ ]

iii) Upi ni umoja wa neno **madoa** kati ya haya?
(a) Madoa (b) Madoadoa (c) Doa
(d) Vidoadoa (e) Midoa [ ]

iv) Wazazi wa Ranginyingi wameaga dunia. Bainisha maana ya nahau **aga dunia**.
(a) Safiri (b) Kufariki (c) Kuzimia
(d) Kuishi milele (e) Kuishi maisha mabaya [ ]

v) Unadhani ni nani anayeongelewa katika hadithi hii?
(a) Kinyonga (b) Kipepeo (c) Babu
(d) Kobe (e) Nungunungu [ ]

2. Chagua herufi ya jibu sahihi kisha andika kwenye kisanduku ulichopewa.

i) Jibu lipi linategua kitendawili, "Pita huko na mimi nipite huku tukutane kwa mjomba".
(a) Majani (b) Maji (c) Mkanda
(d) Reli (e) Barabara [ ]

ii) Kitendawili kipi kinateguliwa na picha hii? 4



(a) Chai yangu iko shambani.
(b) Ubwabwa wa mwana mtamu.
(c) Watoto wa tajiri wanatembea bila nguo.
(d) Ninakunywa mchuzi nyama natema.
(e) Kisima changu siku zote hakikosi maji. [ ]

iii) Babu Koya alikuwa anayumbayumba kwa sababu alikuwa amepiga maji. Nahau **piga maji** inafanana na ipi kati ya hizi? (a) Piga mtindi (b) Piga mwayo
(c) Piga kasia (d) Piga pasi (e) Lewa pombe [ ]

iv) Mwalimu atacheza na watoto. Je, sentensi hii itaonekanaje katika hali ya mazoea?
(a) Mwalimu hatacheza na watoto. (b) Mwalimu asingecheza na watoto.
(c) Mwalimu hucheza na watoto. (d) Mwalimu hachezi na watoto.
(e) Mwalimu alicheza na watoto. [ ]

v) Johari alinunua <u>koroboi</u> kubwa dukani. Kisawe cha neno lililopigiwa mstari ni kipi?
(a) Mwanga (b) Chemli (c) Kibatari (d) Kuni (e) Taa ya umeme [ ]

vi) Bainisha kiambishi cha nafsi katika neno lililokolezwa cha sentensi, "Wanafunzi **waliimba** wimbo mzuri".
(a) Wa - (b) - na - (c) - wa (d) li - (e) - mba [ ]

vii) Ndege huishi kwenye kiota, binadamu huishi kwenye nyumba. Je, jina jingine la maeneo hayo huitwaje? (a) Makazi (b) Nyumbani
(c) Jengoni (d) Mazingira (e) Zizini [ ]

viii) Mwalimu wa Kiswahili hupenda kutusimulia hadithi darasani. Jina lipi unaweza kutuita sisi wasikilizaji wa hadithi? (a) Wazungumzaji (b) Fanani
(c) Hadhira (d) Hadhara (e) Hadithi [ ]

ix) "Umesahau daftari lako la Kiswahili darasani". Sofia alimwambia Ummy. Hii ni aina gani ya kauli? (a) Kauli ya kutendwa (b) Kauli taarifa (c) Kauli ya kutendeana
(d) Kauli halisi (e) Kauli ya kutenda [ ]

x) Mkulima alilima shamba la viazi. Katika mtiririko wa aina za maneno, sentensi hii itaonekanaje? (a) T+ TS +N+HS+N (b) N+T+N+H+N
(c) N+T+N+H+E (d) N+T+N+E+E (e) TS+N+H+E+N [ ]

CamScanner

3. **Oanisha maneno ya Orodha A na Orodha B kwa kuandika herufi ya jibu sahihi kwenye kisanduku.**

Orodha A			Orodha B
i)	Ahidi	[ ]	A. Elimu au ujuzi aupatao mtu kutokana na kusoma, kusikia au kutenda.
ii)	Nidhamu	[ ]	B. Ukumbi maalumu wa kulia chakula.
iii)	Zuru	[ ]	C. Hali ya mtu kuwa mwema.
iv)	Maarifa	[ ]	D. Nenda mahali kwa madhumuni ya kutembelea, kujifunza jambo au kuona kitu.
v)	Bwalo	[ ]	E. Weka dhamira ya kutekeleza jambo fulani.
			F. Tabia njema aliyonayo mtu katika jamii anayoishi.

SEHEMU B: (Alama 20)

4. **Kamilisha methali zifuatazo kwa kuandika jibu sahihi katika kipengele i -v.**

i) Maneno ni daraja _____

ii) Mfukuzwa kwao _____

iii) Jiwe la kutupa ngomani _____

iv) _____ ukienda haurudi.

v) _____ mtii.

5. **Soma shairi lifuatalo kisha jibu maswali yanayofuata.**

Msituni nikakuta, nyuki wamo mizingani,
Kwa juhudi wanakita, mara nje mara ndani,
Husuda wameikata, hata hawaseng'enyani,
Nyuki ni wadudu duni, wanashinda kwa umoja.

Mchwa nao nikaona, wamejenga maskani,
Wafanya bidii sana, uvivu hawatamani,
Wao husaidiana, tena hawadanganyani,
Mchwa wadudu wa chini, wanaishi kwa umoja.

CamScanner

Nao jeshi la siafu, hutandawaa njiani,

Wanakwenda bila hofu, maana wajiamini,

Silaha zao dhaifu, meno tena hawaoni,

Wa kusaidia nani, kwani wanao umoja.

Nao chungu wachukuzi, Nyamarima wa njiani,

Masikini wapagazi, mizigo yao kichwani,

Ingawa si wachokozi, wakali ukiwahini,

Katu hawafarakani, uanadamu kwa umoja.

Maswali;

i) Je, shairi hili lina beti ngapi?_____

ii) Mtunzi wa shairi anajulikana kama nani kishairi?_____

iii) Mshororo wa tatu katika ubeti wa pili una mizani mingapi?_____

iv) Shairi hili linahimiza nini?_____

v) Andika nahau moja inayoendana na shairi hili _____

SEHEMU C: (Alama 10)
Jibu swali la sita

6. Tumia maneno kwenye kisanduku kuandika tangazo kwa mtiririko unaofaa.

Nunua vitabu bora, Mzazi au mlezi, Vitabu bora kwa elimu bora
Tunapatikana Dar es Salaam, Barua pepe, director general@tiego.tz.

(i) _____

(ii) _____

(iii) _____

(iv) _____

(v) _____

CamScanner